# STANDARD SIX YEAR 2016

# END-TERM 2,

**KISWAHILI PAPER**

**TIME: 1HR-40MINS**

Coordinated by KENPRO,
Macjo Arcade, 4th Floor, Suite 15E,
Off Magadi Road, Ongata Rongai |Tel: +254202319748 |
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website:www.schoolsnetkenya.com

# KISWAHILI TIME: 1HR 40MINS

**Chagua jibu sahihi kati ya yale uliyopewa kujaza nafasi zilizoachwa wazi.**

Kuku ____1____ ____2____ akidona mpunga alianguka ____3____ akafa. Walipomwangalia mwili ____4____ ____5____ ulijaa sungusungu. ____6____ kuku aliyekufa ____7____ alichukua wakati ____8____ kukiri kuwa ndiye ____9____. Alimgeuza ili kubainisha ____10____ lakini hakupata ____11____. Akiwa na hasira ____12____ alifululiza ____13____ hadi sokoni ____14____ kumnunua kuku ____15____.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. moja | B. mbili | C. mmoja | D. hiyo |
| 2. | A. iliyokuwa | B. aliyekuwa | C. kulichokuwa | D. kilivyokuwa |
| 3. | A. chini | B. jini | C. juu | D. kweli |
| 4. | A. yake | B kwake | C. wake | D. chake |
| 5. | A. kote | B. wote | C. yote | D. pote |
| 6. | A. Kwenye | B. Penye | C. Wenye | D. Mwenye |
| 7. | A. hapo | B. pale | C. humo | D. huko |
| 8. | A. mrefu | B. ndefu | C. refu | D. sana |
| 9. | A. hasa | B. yeye | C. yake | D. mwenyewe |
| 10. | A. kilichomwua | B. kilichomuwa | C. kilimua | D. kilichomwuua |
| 11. | A. popote | B. zozote | C. lolote | D. yeyote |
| 12. | A. nyingi | B. mwingi | C. kingi | D. vile |
| 13. | A. safari | B. hatua | C. mwendo | D. mguu |
| 14. | A. ili | B. kwa | C. ndipo | D. ilipo |
| 15. | A. tena | B. mwengine | C. wote | D. ingine |

**Kuanzia swali la 16-30 chagua jibu sahihi**

16. Jina jingine la ukuta ni ____
A. ukumbi
B. kiambaza
C. kuta
D. msonge

17. **Tambua maana ya istiara:**
Juma ni lami ____
A. mweusi tititi
B. mweupe pepepe
C. ni mjanja
D. ni mlafi



Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

18. Mvua _______________ sana.

A. umenyesha

B. imenyesha

C. amenyesha

D. kumenyesha

19. Mahali hapa _______________ uchafu mwingi.

A. ina B. kuna

C. pana D. mna

20. Nyama ya mgongo huitwa _____________?

A. kidari B. fisi

C. ndewe D. sarara

21. Ni gani kati ya majibu haya ni thumni ni _______?

A. $^1/_3$ B. $^1/_4$

C. $^1/_9$ D. $^1/_8$

22. Tunasema ___________ la wazee.

A. shamba B. baraza

C. darasa D. jamii

23. **Teua kitenzi katika haya uliyopewa.**

A. kondoo B. cheka

C. shuleni D. daftari

24. **Kamilisha methali:**

Akili ni nywele __________

A. ukipewa usikatae

B. haina matata

C. kila mtu ana zake

D. huondoa maarifa

25. Ni upi msamiati wa hospitalini?

A. kalamu

B. uyoka

C. upawa

D. chepeo

26. **Chagua wingi**

Simu yako ni hii.

A. Simu zako ni hizi.

B. Simu zenu ni hizi.

C. Masimu zenu ni hizi.

D. Simu zenu ni hizi.

27. Neno **mlango** liko katika ngeli gani?

A. A - WA B. KI - VI

C. U - I D. YA - YA

28. Mtoto aliyefiwa na wavyele wake wote anaitwaje?

A. Kizuka B. kivyere

C. yatima D. mlalahoi

29. **Kanusha:**

Nimekuona

A. Nilikuona B. Sikukuona

C. Nitakuona D. Sijakuona

30. **Tambua kinyume cha sentensi ifuatayo:**

Alipowasili nilikuwa nimeondoka

A. Alipowasili nilikuwa nimeondoka

B. Alipowasili nilikuwa nimerudi

C. Alipoondoka nilikuwa nimewasili

D. Alipowasili sikuwa nimeondoka

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40**

Dunia imejaa uhasama. Ni bayana kwamba hakuna usalama unaowazunguka na kuwalinda wananchi wa taifa lolote lole. Unapofungua redio kusikiliza taarifa ya habari, dondo zinazokufika ni za kutia wasiwasi na taharuki. Mara ujambazi, mara vita. Hakuna utulivu wa tulituli.

Hivi karibuni kumetokea habari za kusikitisha abadan katan katika jimbo la Darfur nchini Sudan, uhasama unaotendewa waja si wa kuambilika wala kusemezeka. Watoto malaika wa Mungu wanateseka kwa madhili wasiyoelewa fika. Akina mama wanatendewa unyama nanduli hayawani waroho. Hata ikiwa amani haiji ila kwa ncha ya upanga si haki kuwatendea waja jinsi hivyo.

Huko Burundi. wakimbizi waliokimbilia usalama wao walijipata kwenye mikasa na visa vya **kuatua roho zao.** Mbona waasi wasio na uhesani. Kuwalenga mitutu ya bunduki na kuwatupa jongomenu? Je, tutafanya nini ili kuufanya ulimwengu uwe salama wa kukalika raha mustarehe? Umoja wa mataifa **unawapigia mbiu hawasikii.**

Madola yenye uwezo kama Amerika yanapiga na kujitanua vifua kuwa yana uwezo wa kivita. Lakini wapi: Huko Iraki waliwasha moto waziweze kuuzima. Lililobaki ni wananchi wa msafu walionyang'anywa uhuru wa demokrasia. Unaotekelezwa si wa haki bali ubepari wa kiimla.

31. Majanga yanayotulia usalama wa binadamu duniani yanadhihilishwa na_____
    A. zilizala
    B. visa na mikasa kila uchao
    C. balaa na vurumai
    D. upujaji wa mali
32. Kuenea kwa uadui duniani kumekua kiasi kwamba
    A. usalama haupatikani popote
    B. amani haipo kamwe
    C. barabara zote hazipitiki
    D. waja wamepotea
33. Kulingana na taarifa uliyosoma_______
    A. matangazo yanasababisha taharuki kubwa
    B. matangazo yanazua zogo vijijini
    C. matangazo yanafafanua chimbuko la uhasama
    D. matangazo yanawatia moyo wahusika
34. Visa vya watoto kuteseka vilipatikana wapi?
    A. Nchini Darfu, Sudan
    B. Mjini Sudan, Burundi
    C. Mjini Darfur, Sudan
    D. Nchini Marekani kwa Iraq
35. Ni nini kilichoripotiwa nchini Burundi?
    A. Ufyatulianaji wa risasi
    B. Mauaji ya wakimbizi
    C. Maafa ya wazalendo
    D. Utensi wa mawaziri
36. Tamaa ya mwandishi ni kuona ulimwengu ambao watu wanaishi_______
    A. raha na karaha
    B. raha mustarehe
    C. tengo tahani
    D. raha na ving'ong'o
37. Visa vilivyowatua roho zao viliwaaha wakiwa____
    A. wamezubaa na kupumbaa
    B. mahututi na maiti
    C. wanyonge na wadhaifu
    D. wanga na wajasiri
38. Kwa mujibu wa habari, wanaojidai kuwa na uwezo ni pamoja na__________
    A. Amerika
    B. Emuko
    C. Iraki
    D. Burundi
39. Je, kwa demokrasia ulimwenguni?
    A. La waja wanateseka popote walipo
    B. Ndiyo, kwa ushahidi wa Mwamerika
    C. La hasha! Badala yake kwanza sera za kiimla
    D. La! Demokrasia ipo Amerika na Iraki
40. Kifungu ulichokisoma kinaangazia nini?
    A. kilio cha wasiokuwa na usalama
    B. Utetesi juu ya ukosefu wa usalama
    C. Tetesi juu ya usalama ulimwenguni
    D. Upungufu wa demokrasia marekani

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41-50**

Neno ukimwi lina maana ya Ukosefu wa Kinga mwilini. Huu ni uele ambao umekuwa ukisumbua binadamu kwa mika na mikaka, maadamu hauna tiba kwa jinsi ulivyo sugu kwani hausikii dawa wala kafara. Maradhi haya aghalabu huambukizwa kutoka kwa mhusika kupitia njia kadha kama vile ngono au mzazi mhasiriwa kumwambukiza mtoto anapokuwa akijifungua. Aidha mgonjwa anayehitaji damu anapotiwa damu huenda ikawa ina viini vya ugonjwa huu. Mbali na hayo, waja wanaoshiriki vifaa vya makali kama vile nyembe, makasi au hata visu wakati wa tohara, huweza kuambukizwa kwa haraka.

Athari za ukongo huu ni za kusikitisha mno. Unyende! Kanisa! Siahi! Kila kijini ni **kilio cha mauko**. Wanawakiwa tumbi nzima wametapakaa kote vitongojini. Watoto hawa ambao sasa ni mayatima hubaki matesoni bila chakula makao maalum, mavazi wala elimu. Ndoto zao za usoni huagana nazo wakameza mrututu. Maisha kwao huwa kitendawili ambacho kujaribu kukitegua ni kama kutaka kupigana na papa au nyangumi. Hawana rafiki wala mhisani kiasi kwamba msemo wa wazee eti akufaaye kwa dhikindiye rafiki. Kwao ni chungu zaidi ya shubiri.

41. Neno Ukimwi lina maana ya ______
 A. Ukosefu wa kiingilio mwilini
 B. Ukosefu wa tabia
 C. Ukosefu wa kinga mwilini
 D. Ukosefu wa dawa mwilini

42. Ugonjwa pia huitwa ______
 A. uele
 B. Umaskini
 C. Ufukara
 D. Ukosefu

43. Je, mtu anaweza kuambukizwa Ukimwi bila kushiriki ngono?
 A. ndiyo B. la
 C. la hasha D. haiwezekani

44. Kulingana na taarifa inaelekea kuwa ni heri ____
 A. kutoshiriki tohara kitamaduni
 B. kushiriki tohara kitamaduni
 C. kuishi pamoja watu wengi
 D. kunyoa ndevu zako nyumbani

45. Mtoto aliye tumboni anaweza kuwa na virusi kwa njia gani?
 A. Mama anapojifungua
 B. Mama anapopata mimba
 C. Mama anapomnyonyesha
 D. Anaponyolewa kwa wembe mpya

46. Suala la Ukimwi linasababisha ______
 A. kilio
 B. raha
 C. kicheko
 D. anasa

47. Kwa nini kukabiliana na maisha kwa raha ni kama kupigana na nyangumi?
 A. ni rahisi
 B. si jambo rahisi
 C. ni sawa
 D. hatujaambiwa

48. Wanawakiwa ni sawa na ______
 A. wenye mali
 B. mabwenyenye
 C. mayatima
 D. mabalozi

49. Akufaaye kwa dhiki ndiye ______
 A. mwenyewe B. rafiki
 C. mzazi D. adui

50. Kichwa mwafaka kwa habari hii ni ____
 A. Ukimwi
 B. Watu wenye tabia mbaya
 C. Maambukizi ya ngono
 D. Maradhi mbalimbali



Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27